# Uchakataji wa taarifa binafsi za watu waliopendekezwa kufika Ufini kama wakimbizi wanaopewa makazi mapya

Nchini Ufini Idara ya Uhamiaji inachakata taarifa binafsi za wakimbizi wanaopewa makazi mapya ndani ya mfumo wa uchakataji wa masuala ya watu wa nchi za kigeni (UMA). Huo mfumo ni rejista ya wenye mamlaka, inayosimamiwa na kutumiwa kwa mfano kwa ajili ya ukaaji wa watu wa nchi za kigeni na ufanyaji maamuzi.

Wenye mamlaka wanaochakata taarifa binafsi zako wana jukumu la usiri, na hawaruhusiwi kufichua taarifa zinazopaswa kuhifadhiwa siri, kama vile taarifa binafsi. Jukumu la usiri linafuatwa kila wakati, hata baada ya kazi na baada ya ajira kuisha.

Taratibu zinazoelezwa na mwongozo zinahusika na uchakataji wa uamuzi wa kukubali pamoja na kukataa.

**Taarifa binafsi ni jambo gani?**

Taarifa binafsi ni taarifa zote zinazohusika na mtu aliyetambuliwa au anayeweza kutambuliwa. Taarifa binafsi ni aina za taarifa ambazo zinaweza kutumiwa kwa msingi kwa kumtambua mtu moja kwa moja au kwa njia isiyo ya moja kwa moja, kwa mfano kwa njia ya kuunganisha taarifa moja kwa taarifa nyingine, inayowezesha utambuaji. Kwa mfano mtu anaweza kutambuliwa kupitia jina lake, namba ya utambulisho au sifa bainifu fulani.

## Jinsi gani wenye mamlaka wanatumia taarifa zako binafsi?

### Maana ya uchakataji wa taarifa

Shirika la Umoja wa Mataifa la kuhudumia Wakimbizi UNHCR limetoa pendekezo kwa nchi ya Ufini, kwamba uchaguliwe kama mkimbizi wa kupewa makazi mapya nchini Ufini na limewasilisha taarifa zako kwa Idara ya Uhamiaji. Kwa msingi wa taarifa hizo Idara ya Uhamiaji inajitahidi kuhakikisha kama kuna vigezo vya kisheria (Sheria ya Wageni 301/2004), ili nchi ya Ufini iweze kuangalia, kama unaweza kupewa hadhi ya ukimbizi na haki ya makazi nchini Ufini.

Wenye mamlaka katika Idara ya Uhamiaji, Vituo vya Maendeleo ya Kiuchumi, manispaa na kwenye Huduma za Ustawi wa Jamii na Afya za Majimbo wanatumia taarifa hizo pia katika utoaji wa nafasi za makazi kwenye manispaa kwa wakimbizi ambao wamekubaliwa kupewa makazi mapya nchini Ufini kwa mujibu wa majukumu yao ya kisheria. (Sheria juu ya ukuzaji wa huduma za ujumuishaji wa wahamiaji 1386/2010). Aidha Shirika la Umoja wa Mataifa la Uhamaji (IOM) na Shirika la Msalaba Mwekundu la Ufini (SPR) yanatumia taarifa hizo katika maandalizi ya safari kulingana na mikataba iliyofanyika baina ya Idara ya Uhamiaji na IOM na SPR kuhusu huduma za upokeaji wa wakimbizi wanaopewa makazi mapya.

Uchakataji wa hizo taarifa inahitajika kwa ajili ya kutimiza majukumu ya kisheria ya msimamizi wa usajili. Uchakataji unafanyika kwa mujibu wa ibara ya 1 c ya kifungu cha 6 cha Sheria ya Ulinzi wa Data ya Jumuiya ya Ulaya (EU) 2016/679.

## Vyanzo vya taarifa – Idara ya Uhamiaji inapata taarifa zako kutoka wapi?

Idara ya Uhamiaji inapata taarifa binafsi na za kifamilia pamoja na taarifa juu ya sababu za ukimbizi, juu ya mahitaji ya kupewa makazi mapya pamoja na mahitaji maalum yanayoweza kuwepo kuhusu hali, afya au mahusiano ya kifamilia kupitia fomu za taarifa binafsi za UNHCR. Aidha kwa kusudi maalum Idara ya Uhamiaji inapata ithibati au nyaraka zinazohusiana na afya au manufaa ya mtoto za wakimbizi waliopendekezwa kupewa makazi mapya kutoka kwa UNHCR pamoja na waraka wa taarifa za afya kutoka kwa IOM.

## Wapokeaji wa Taarifa zako binafsi

Kama hutachaguliwa kama mkimbizi anayepewa makazi mapya nchini Ufini, Idara ya Uhamiaji haitagawa taarifa zako.

Kama utachaguliwa kama mkimbizi anayepewa makazi mapya nchini Ufini, wenye mamlaka katika Idara ya Uhamiaji, kwenye Vituo vya Maendeleo ya Kiuchumi vya kieneo, kwenye Huduma za Ustawi wa Jamii na Afya za Jimbo na kwenye manispaa ihusikayo na upokeaji wana haki ya kuona na kuchakata taarifa zako zilizohifadhiwa kwenye mfumo wa uchakataji wa masuala ya watu wa nchi za kigeni kwa kuzingatia mipaka ya mamlaka yao. Aidha Idara ya Uhamiaji inakabidhi taarifa kwa mashirika ya IOM na SPR yanayoshirikiana na Idara ya Uhamiaji katika maandalizi ya usafiri, yanayochakata taarifa pamoja na wanakandarasi wao kuhusiana na maandalizi ya safari.

## Uhamishaji wa taarifa zako nje ya eneo la EU au ETA

Idara ya Uhamiaji inaweza kuhamisha taarifa zako binafsi kwa IOM kwa mujibu wa mkataba wa Idara ya Uhamiaji na IOM juu ya huduma zinazotolewa katika upokeaji wa wakimbizi wanaopewa makazi mapya.

## Nyakati za uhifadhi wa taarifa binafsi kwenye mfumo wa uchakataji wa masuala ya watu wa nchi za kigeni

Taarifa zinazomhusu msajiliwa zitafutwa, wakati uhitaji wa kuzitumia haupo tena, na mwisho baada ya miaka kumi kupita baada ya ingizo la mwisho ambalo linamhusu msajiliwa. Taarifa zilizofutwa zinahifadhiwa kwa kudumu kwa njia ya kielektroniki peke yake kwa mujibu wa uamuzi wa Idara ya Hifadhi ya Kumbukumbu Tuli.

Taarifa zilizotunzwa kwenye hifadhi ya kumbukumbu tuli, zinaweza kutafutwa kutoka mfumo wa uchakataji wa masuala ya watu wa nchi za kigeni kwa kuzingatia mipaka pekee ya upatikanaji wa haki za matumizi.

# Unaweza kukagua taarifa zako binafsi

## Haki ya kufikia taarifa zako binafsi

Idara ya Uhamiaji ni msimamizi wa masjala ya mfumo wa uchakataji wa masuala ya watu wa nchi za kigeni. Una haki ya kupata uthibitisho kutoka kwa msimamizi wa masjala, kama mwenye mamlaka anachakata taarifa binafsi zinazokuhusu, au hazichakati. Kama mwenye mamlaka anachakata hizo taarifa binafsi, una haki ya kufikia taarifa zako binafsi. Msimamizi wa masjala anaweza kunyima haki ya kukagua katika kesi mahususi pekee. Kupitia ombi una haki kupata kuona taarifa zako binafsi zilizohifadhiwa na zinazochakatwa, kwa kuwasilisha ombi kuhusu hilo suala kwa wakala ya Idara ya Uhamiaji au masjala kwa kutumia anwani ya migri@migri.fi anwani ya posta ya SLP 10, 00086 Idara ya Uhamiaji.

## Haki ya kurekebisha au kuongeza taarifa

Kama unagundua kwamba taarifa zako zina upungufu au makosa, unaweza kuomba zirekebishwe. Katika hali kama hiyo tunakuomba kueleza taarifa gani ina makosa na kutoa misingi yako juu ya makosa. Eleza pia, jinsi gani taarifa zingestahili kubadilishwa, au taarifa gani ingepaswa kuongezwa na namna gani.

## Ujumbe juu ya uchakataji wa Taarifa binafsi na haki ya kutoa malalamiko kwa mamlaka ya usimamizi

Kama unataka kutoa ujumbe juu ya tatizo linalohusika na uchakataji wa taarifa zako binafsi, kimsingi wasiliana na mwakilishi wa msimamizi wa masjala/Afisa wa Ulinzi wa Data (taarifa za mawasiliano hapo chini). Una haki ya kutoa malalamiko juu ya uchakataji wa taarifa zako binafsi kwa mamlaka ya usimamizi pia. Nchini Ufini mamlaka ya usimamizi ni Kamishna wa Ulinzi wa Data. Tovuti ya mtandao ya Kamishna wa Ulinzi wa Data inapatikana kwenye anwani ya www.tietosuoja.fi.